
# JINSI YA KUPATA AMRI YA ULINZI



Imetolewa na Ofisi ya Utawala wa Mahakama

# Amri za Ulinzi

Ofisi ya Utawala wa Mahakama inapenda kutoa mwongozo huu wa jinsi ya kupata amri za kiraia kwa wale wanaoomba ulinzi dhidi ya unyanyasaji na ukatili wa majumbani, ukatili na unyanyasaji wa kimapenzi, kunyemelea na shambulio la kingono. Tafadhali kumbuka kwamba mlalamikaji ni mtu ambaye anawasilisha ombi kwa ajili ya amri ya ulinzi. Mshtakiwa ni mtu ambaye anatuhumiwa kufanya unyanyasaji.

## 1. Kuna aina gani za Amri za Ulinzi?

Mahakama inaweza kutoa amri ya ulinzi kwa muathirika wa ukatili wa majumbani, ukatili na unyanyasaji wa kimapenzi, kunyemelea na/au shambulio la kingono. Mashauri ya amri za ulinzi ni tofauti na mashauri ya jinai. Amri za ulinzi zinalenga kuzuia matendo ya baadaye ya ukatili na unyanyasaji. Shauri la jinai kwa kawaida hushughulikiwa na mwanasheria wa wilaya, ambaye humshtaki mshtakiwa kwa matendo ya ukatili na unyanyasaji ambayo tayari yamefanyika.

**Amri za Ulinzi za Muda Mfupi**. Mahakama inaweza kutoa amri ya dharura ya ulinzi (Emergency Protective Order, EPO) katika mashauri ya ukatili wa majumbani au amri ya ulinzi ya mtu na mtu ya muda mfupi (Temporary Interpersonal Protective Order, TIPO) katika mashauri ya ukatili wa kimapenzi na unyemeleaji/shambulio la kingono. Hizi ni amri za muda mfupi zinazolenga kuzuia ukatili na unyanyasaji kwa kuweka vikwazo kwenye matendo ya mshtakiwa hadi usikilizaji wa mashauri ufanywe na mahakama, kwa kawaida ndani ya siku 14.

**Amri za Ulinzi za Muda Mrefu.** Amri za ukatili wa majumbani (Domestic Violence Order, DVO) na amri za ulinzi kati ya mtu na mtu (Interpersonal Protective Order, IPO) zinaweza kudumu hadi miaka mitatu. Amri hizi zinalenga kuzuia unyanyasaji na ukatili kwa kumwekea vikwazo mshtakiwa baada ya usikilizaji wa shauri mahakamani.

## 2. Kwa nini unaomba amri ya ulinzi wa ukatili wa majumbani (DVO) au Ulinzi wa baina ya mtu na mtu (IPO)?

Kuwa na sifa ya kuwasilisha DVO au IPO, mshtakiwa lazima awe amefanya moja kati ya yafuatayo:

- Amekujeruhi au amekushambulia wewe au mtoto.
- Amekukaba wewe au mtoto.

- Amekunyanyasa kingono au amekushambulia kingono wewe au mtoto.
- Amekutishia kukujeruhi au kukushambulia wewe au mtoto.
- Amekunyemelea wewe au mtoto.
- Amefanya kitu ambacho kinakufanya wewe au mtoto awe katika hatari ya kujeruhiwa, kujeruhiwa vibaya, unyanyasaji wa kijinsia, ukabaji, au shambulio.
- Amemnyanyasa mnyama wa nyumbani kama njia ya kulazimisha, kudhibiti, kuadhibu, kutishia, au kulipiza kisasi dhidi yako au mtoto.
- Amefanya kitu ambacho kinakufanya wewe au mtoto kuwa na woga wa unyanyasaji wa mnyama wa nyumbani kwa wakati huo kama njia ya kulazimisha, kudhibiti, kuadhibu, kutishia, au kulipiza kisasi dhidi yako au mtoto.

## 3. Je, nani anaweza kupata amri ya ulinzi?

Ili kupata amri ya ulinzi, wahusika lazima wawe na uhusiano unaostahiki. Uhusiano unaostahiki ni pamoja na:

- Wanafamilia. Hii inajumuisha mwenza, mwenza wa zamani, mzazi, mtoto, mtoto wa kambo, babu/bibi, mjukuu, au mtu mwingine yeyote anayeishi katika kaya hiyihiyo kama mtoto ikiwa mtoto huyo ndiye anayedaiwa kuathirika.
- Jamaa wa wenza ambao hawajaoana. Hii inajumuisha jamaa wa wenza ambao hawajaoana ambao wanadaiwa kuwa na mtoto pamoja, watoto wowote wa wenza hao, au jamaa wa wenza ambao hawajaoana ambao wanaishi pamoja au waliishi pamoja hapo kabla.
- Uhusiano wa uchumba kati ya watu wawili ambao wana au walikuwa na uhusiano wa kimapenzi au wa uhusiano wa karibu.
- Mwathirika wa kunyemelea au shambulio la kingono.

## 4. Je, nani anayeweza kulindwa?

- Unaweza kuomba ulinzi kwa ajili yako mwenyewe, watoto wako na/au watu wengine ambao unadhani wanaweza kuhitaji ulinzi.
- Kama wewe ni mtu mzima na unadhani mtoto anahitaji ulinzi lakini wewe huhitaji, unaweza kuwasilisha ombi kwa niaba ya mtoto huyo.

- Ikiwa una umri chini ya miaka 18, mtu mzima anaweza kuwasilisha ombi kwa niaba yako.

- KUMBUKA: Unaweza pia kuiomba mahakama uweze Kumiliki wanyama wa nyumbani unaomiliki pamoja na mtu mwingine ambao wamekuwa wakipata vitisho au madhara.

## 5. Je, wapi ninaweza kuwasilisha ombi la amri ya ulinzi?

Kuwasilisha ombi la amri ya ulinzi, tembelea Ofisi ya Karani wa Mahakama kwenye wilaya ya nyumbani au kwenye wilaya ambayo unaishi kwa sasa ikiwa umeondoka nyumbani kwako ili kukimbia unyanyasaji.

Kuna Ofisi ya Karani wa Mahakama ya Mzunguko katika kila wilaya ya Kentucky. Kwa taarifa za mawasiliano ya Ofisi zote 120 za Mahakama ya Mzunguko, tembelea:

**https://kycourts.gov/Courts/County-Information/Pages/default.aspx**

- Unaweza kupata amri ya ulinzi saa 24 kwa siku.

- Hakuna ada au gharama za kuwasilisha ombi.

- Baada ya muda wa kazi, unapaswa kuwasiliana na afisa usalama wa mahali ulipo kwa msaada wa kupata amri ya ulinzi.

- Inapendekezwa kwamba uwasiliane pia na mpango wa ukatili wa majumbani katika eneo lako - wanaweza kukusaidia katika utaratibu wa kupata amri ya ulinzi saa za kazi na hata baada ya saa za kazi. Baadhi ya makazi ya dharura yanaweza kutuma malalamiko kwa njia ya mtandao. Muungano wa Kentucky Dhidi ya Ukatili wa Majumbani (The Kentucky Coalition Against Domestic Violence) Una makazi ya dharura jimboni kote. Ramani ya maeneo na taarifa za mawasiliano zipo kwenye ukurasa wa 10.

## 6. Je, ninajazaje fomu za malalamiko?

Utaombwa kutoa taarifa zako na za mshtakiwa. Ni muhimu kutoa taarifa nyingi za mshtakiwa kadri iwezekanavyo – kama vile tarehe ya kuzaliwa, namba ya Hifadhi ya Jamii na anwani – ili aweze kupewa amri yoyote inayoweza kutolewa. Anwani yako na tarehe ya kuzaliwa zitakuwa siri.

Utaombwa uorodheshe watoto wowote ambao wewe na mshtakiwa mnao, na unaweza kuomba kwamba watoto hawa walindwe na amri yoyote inayoweza kutolewa.

Kama unahitaji umiliki wa mnyama wa nyumbani unayemmiliki pamoja na mtu mwingine, toa maelezo ya utambulisho ya mnyama/wanyama huyo/hao.

Chini ya "Hoja ya Kupata Ruhusa", unaweza kuomba ulinzi ambao unadhani unafaa katika mazingira yako. Angalia Swali Namba 9 ili kupata mfano wa vipengele vinavyoweza kujumuishwa katika amri ya ulinzi.

Mwishoni mwa malalamiko, utaombwa kuapa kwamba taarifa unazotoa ni za kweli.

Mahakama ya Haki ya Kentucky inatoa mwongozo wa mahojiano ya mtandaoni (kwa sasa yanafanyika kwa Lugha ya Kiingereza tu) ambao husaidia kukamilisha malalamiko kwa kutumia mfululizo wa maswali ya mahojiano. Unaweza kupata programu hiyo, au nyenzo nyingine za kisheria za kujisaidia mwenyewe kwa kutumia kiunganishi hiki:

https://kycourts.gov/Legal-Help/Pages/default.aspx.

## 7. Je, nini kitatokea baada ya ombi kuwasilishwa?

Malalamiko yatawasilishwa kwa hakimu au kamishna wa kesi mara moja ili kuamua kama tuhuma zinahitaji amri ya muda kutolewa. Hakimu pia anapitia tuhuma ili kubaini kama zimefikia tafsiri ya ukatili wa majumbani na unyanyasaji, unyanyasaji na ukatili wa kimapenzi, shambulio la kingono, au unyemeleaji.

Hakimu atatoa amri ya muda ya ulinzi (EPO au TIPO) kama tuhuma zilizotolewa kwenye malalamiko zinaonyesha uwepo wa hatari kwenye muda uliopo. Kama sivyo, mahakama inaweza kutupilia mbali malalamiko au kutoa wito kwa ajili ya usikilizaji rasmi wa shauri lako ili kuamua kama amri ya ulinzi ya muda mrefu inastahiki.

Ikiwa hakimu atatoa EPO, TIPO au wito, usikilizaji wa shauri utapangwa ndani ya siku 14 ili kuamua kama amri ya muda mrefu inahitajika. Utapewa hati ambayo itakuonyesha tarehe na muda wa kusikiliza shauri hilo. Kama hujui shauri lako litasikilizwa lini, wasiliana na Ofisi ya Karani wa Mahakama ya Mzunguko katika wilaya uliyowasilisha malalamiko yako.

Afisa usalama atajaribu kumpatia amri ya ulinzi au wito mshtakiwa. Amri ya ulinzi haiwezi kufanya kazi hadi mshtakiwa atakapopewa nakala ya amri au atakapojulishwa kuhusu amri ya ulinzi na afisa usalama. Unaweza kuwasiliana na "agency assigned service" (aliyeorodheshwa kwenye amri) ili kujua kama mshtakiwa amepewa nakala.

Amri ya ulinzi (EPO/TIPO) itafanya kazi hadi pale usikilizaji wa shauri mahakamani umefanyika, kwa kawaida ndani ya siku 14. Kama mshtakiwa hajapewa EPO/TIPO, amri itaendelea hadi huduma itakapotekelezwa (hadi miezi sita) au hadi pale amri itakapoondolewa  na mahakama. Hata kama unadhani huhitaji tena ulinzi, utatakiwa uhudhurie siku iliyopangwa ya usikilizaji wa shauri mahakamani.

Hakimu pekee ndiye anayeweza kutoa tarehe mpya ya mahakama au kubadili amri. Kuliongana na hali za shauri, mahakama inaweza kukupa udhuru wa kuhudhuria mahakamani siku zijazo hadi pale mshtakiwa atakapopewa nakala. Kama EPO/TIPO haijatolewa kwa hadi miezi sita, utapokea tangazo kutoka mahakamani kwenye anwani yako iliyokuwa inafahamika awali ili kukujulisha kwamba amri inakaribia kwisha na kwamba utatakiwa kuja kwenye Ofisi ya Karani wa Mahakama ili kujaza ombi jipya ili kuendelea na shauri.

## 8. Je, unapaswa kuleta nini katika usikilizaji wa shauri?

Huu unaweza kuwa usikilizaji pekee wa kesi, hivyo unapaswa kuja na mashahidi wowote ulio nao na hati zozote ambazo zinaweza kuwa ushahidi wa kile kilichotokea, kama vile taarifa za polisi, picha na kumbukumbu za matibabu. Kama una ushahidi (ujumbe mfupi, au picha) kwenye simu au kifaa kingine, jaribu kuchapisha ili uweze kuingizwa kwenye kumbukumbu rasmi za mahakama. Kama unataka kuomba shahidi afike, karani wa mahakama ya mzunguko anaweza kukupa fomu za wito wa kisheria mahakamani. Ikiwa unaomba msaada wa mtoto, lete muhtasari wa malipo na mapato ya kodi kama inawezekana. Taarifa zote hizi zitakuwa sehemu ya kumbukumbu ya mahakama.

## 9. Je, nini kinaweza kutokea wakati wa kusikiliza shauri?

Katika usikilizaji kamili wa shauri, mahakama itasikiliza ushahidi kutoka kwako, kwa mshtakiwa na mashahidi wengine wowote. Mahakama inaweza kutupilia mbali shauri au kutoa DVO au IPO (amri ya ukatili wa majumbani au amri ya ulinzi wa mtu binafsi), ambayo inaweza kujumuisha masharti yafuatayo:

1. Kumuamuru mshtakiwa kutowasiliana na wewe au na watu wengine isipokuwa kama ilivyoelekezwa na hakimu.

   **KUMBUKA:** Kama imeombwa na Mlalamikaji, mahakama inaweza kuruhusu kukutana au kuwasiliana mara chache.

2. Kumuamuru Mshtakiwa asiende karibu na makazi yaliyotajwa, shule, au kazini kwa Mlalamikaji.

**KUMBUKA:** Hili lazima liombwe kwenye ombi la amri ya ulinzi. Taarifa yoyote ya anwani iliyotolewa **sio siri** na itaonekana kwa mshtakiwa. Kama itaombwa na Mlalamikaji, mahakama inaweza kumruhusu mshtakiwa kuwa ndani ya futi 500 toka alipo Mlalamikaji katika mazingira yenye ukomo maalum na kwa vigezo maalum.

3. Kumuamuru mshtakiwa kutokukunyanyasa wala kukutisha.

4. Kumuamuru mshtakiwa kutoharibu wala kutozitupa mali zako.

5. Kumuamuru mshtakiwa kuondoka kwenye makazi yako.

   **KUMBUKA:** Amri ya dharura ya ulinzi inaweza kuamuru kwamba kila mmoja pande zote mbili aweze kuchukua vitu vyake binafsi katika makazi waliyokuwa wakikaa kwa pamoja kwa msaada wa vyombo vya usalama, kama itahitajika.

6. Kuruhusu malezi ya muda ya watoto.

7. Kuruhusu kutolewa kwa msaada kwa mtoto/watoto.

8. Kuamuru ushauri nasaha kutolewa.

9. Kumpa mlalamikaji uwezo wa kumiliki mnyama wa nyumbani wa familia.
10. Kitu kingine chochote kinachohitajika kukomesha vitendo vya ukatili siku zijazo.

Unapaswa kusoma kwa makini amri zote unazopewa. Ikiwa una maswali kuhusu amri yako inamaanisha nini, wasiliana na mwanasheria wako (kama unae), mpango wa ukatili wa majumbani wa mahali husika au wakili wa mwathirika.

## 10. Nini kitatokea ikiwa mshtakiwa atakiuka amri ya ulinzi?

Amri ya ulinzi inaweza kutekelezwa katika wilaya yoyote ya jimbo la Kentucky. Majimbo mengine yanaweza kutekeleza amri, lakini inapaswa kusajiliwa katika jimbo lolote ambalo utahamia au unapanga kuishi kwa muda mrefu. Ikiwa mshtakiwa atakiuka amri ya ulinzi, machaguo yako yanaweza kujumuisha:

- Kuwapigia simu polisi, ambao wanaweza kumkamata mshtakiwa.

- Kurudi kwenye mahakama ambayo ilitoa amri ya ulinzi kuomba kwamba mshtakiwa akamatwe kwa dharau ya kukiuka amri hiyo.

- Kurudi kwenye Ofisi ya mwanasheria wa wilaya kuangalia kama mshtakiwa anaweza kushtakiwa kwa kosa la kukiuka amri ya ulinzi.

**Ufuatiliaji wa GPS.** Ikiwa wilaya yako ina huduma ya ufuatiliaji ya mfumo wa upangaji ulimwengu (GPS) iliyopo, unaweza kuiomba mahakama kumuamuru mshtakiwa kuvaa kifaa cha ufuatiliaji wa GPS. Unaweza kufanya hivyo kwa kuwasilisha fomu ya pendekezo mahakamani. Unaweza kuomba fomu hiyo kwenye Ofisi ya Karani wa Mahakama.

Hakimu ataamua kama kumekuwa na ukiukaji mkubwa uliofanywa na mshtakiwa ambao ulihusisha kutokea au kutishia kukudhuru wewe, familia yako, mali zako,au mnyama wa nyumbani. Kama Hakimu atamuamuru mshtakiwa kuvaa kifaa cha kufuatilia mienendo yake, mshtakiwa ataamriwa kulipia gharama za ufuatiliaji anaweza kutakiwa kukivaa kifaa hicho kwa muda wote ambapo amri ya ulinzi itakuwa inafanya kazi.

Ikiwa baadaye utadhani kuwa si muhimu tena, unaweza kuomba kwamba matakwa ya mfumo wa ufuatiliaji GPS yaondolewe.

## 11. Je, ninawezaje kubadilisha au kurefusha amri ya ulinzi?

Ikiwa unahitaji kubadilisha masharti ya amri ya ulinzi, lazima uwasilishe pendekezo la mabadiliko kwenye Ofisi ya Karani wa Mahakama katika wilaya ambayo ulipata amri yako ya ulinzi. Upande wowote unaweza kuwasilisha pendekezo la kurekebisha amri. Kisha hakimu atapitia pendekezo na kufanya uamuzi. Hakimu pekee ndiye anayeweza kubadili baadhi au masharti yote ya amri.

Ikiwa unataka amri ya ulinzi kuongezwa zaidi ya tarehe yake ya mwisho, ni lazima uwasilishe pendekezo mahakamani ambalo linaeleza sababu yako (zako) ya ombi hilo. Pendekezo lazima liwasilishwe kabla ya amri kwisha.

Ikiwa mshtakiwa ameamurishwa kuvaa kifaa cha kufuatilia GPS, unaweza kuomba takwa hilo kurefushwa pia.

## 12. Je, ninawezaje kupata huduma za msaada?

Kama ilivyopendekezwa katika Swali la 5, Muungano wa Kentucky Dhidi ya Ukatili wa Majumbani una makazi ya dharura katika jimbo zima ili kuwahudumia waathirika wa ukatili wa majumbani na ukatili wa baina ya mtu na mtu. Ramani ya maeneo na taarifa za mawasiliano zipo kwenye ukurasa wa 11.

Nakala ya ombi na amri ya ulinzi vitatumwa kwenda kwenye Baraza la Kentucky la Huduma za Afya na Familia (CHFS) na kuelekezwa kwenda ama kwenye Mamlaka ya Huduma za Ulinzi wa Watu Wazima au Mamlaka ya Huduma za Ulinzi wa Mtoto. Mfanyakazi wa ustawi wa jamii kutoka CHFS anaweza kuwasiliana na wewe ili kukupa huduma za msaada. Kupata taarifa zaidi, tembelea www.chfs.ky.gov/Services/.

Ikiwa ni huduma ya bure ya CourtNet kwa wageni inayotolewa na Mahakama ya Haki ya Kentucky, wakati wowote wahanga wanaweza kutafuta matukio ya mahakamani yanayohusiana na kesi zao kupitia hapa https://bit.ly/GuestCourtNet.

Huduma za waathirika pia zinapatikana katika jimbo zima la Kentucky. Kwa taarifa zaidi, piga simu ya bure kwa Namba ya Msaada wa Ukatili wa Majumbani ya Kitaifa (The National Domestic Violence Hotline) 800-799-7233. Pia unaweza kutembelea tovuti www.thehotline.org.

## 13. Je, haki zangu ni zipi chini ya Sheria ya Mwenye Nyumba/Mpangaji?

Ikiwa una amri ya ulinzi iliyotolewa na hakimu, basi unaweza kuwa na haki za ziada chini ya Sheria ya Mwenye Nyumba/Mpangaji, ambayo ilianza kufanya kazi tarehe 29 Juni 2017.

Haki hizi zinatumika tu kwenye mikataba ya upangishaji au ya kupanga iliyoingiwa, au iliyohuishwa, mnamo au baada ya tarehe 29 Juni 2017. Unaweza kutaka kushauriana na mwanasheria au wakili wa mwathirika kwa taarifa za ziada kuhusu haki zako chini ya Sheria ya Mwenye Nyumba/Mpangaji.

**Haki Chini ya Amri ya Ulinzi ya Muda Mfupi au Amri ya Kutowasiliana**

Ikiwa una amri ya ulinzi ya muda mfupi (EPO au TIPO) iliyotolewa au amri ya kutowasiliana iliyotolewa na hakimu kwa mujibu wa KRS 431.064 (shambulio, unyanyashaji wa kingono au ukiukaji wa amri ya ulinzi), una haki zifuatazo:

- Mwenye nyumba hawezi kutamatisha au kushindwa kuhuisha, au kukataa kuingia mkataba wa upangishaji au kodi na wewe (au vinginevyo kukulipiza kisasi) kulingana na matendo ambayo yamekusababishia kupata amri ya ulinzi ya muda mfupi au kulingana na matendo yoyote ambayo yalitokea wakati wa ukiukwaji wa amri ya ulinzi ya muda mfupi.

- Unaweza kubadilisha ufunguo ya kitasa au kubadilisha kitasa chenye ubora uleule wa kitasa au ubora mzuri zaidi. Kwanza, lazima umjulishe mmiliki wa nyumba yako kwamba unadhamiria kubadilisha kitasa na umpatie ufunguo kama atakuomba.

Pia mwenye nyumba anaweza kukataa kutoa ufunguo wa kitasa kipya kwa mshtakiwa hata kama pia ameorodheshwa kwenye mkataba wa upangishaji au wa kupanga.

**Amri za Ulinzi za Muda Mrefu na Utamatishaji wa Mkataba wa Upangishaji**

Zaidi ya haki chini ya amri ya ulinzi ya muda mfupi, mara baada kutolewa kwa DVO au IPO halali dhidi ya mshtakiwa kwa ajili ya ulinzi wako au ulinzi wa mtoto mdogo kwenye kaya yako, unaweza kutamatisha mkataba wa upangishaji au wa kupanga.

Hii haitumiki ikiwa una amri ya ulinzi ya muda mfupi pekee (EPO au TIPO) au amri ya kutowasiliana kwa mujibu wa KRS 431.064. Lazima uwe umepata amri ya ulinzi ya muda mrefu halali (DVO au IPO) kutolewa.

Hii inatumika pekee kwenye mikataba ya upangishaji au kupanga iliyoingiwa au iliyohuishwa mnamo au baada ya tarehe 29 Juni 2017.

**Amri ya Ulinzi ya Muda Mrefu Iliyopatikana Baada ya Kuingia Katika au Kuhuisha Mkataba wa Upangishaji au Kupanga**

Ikiwa ulipata amri yako halali ya ulinzi baada ya kuingia katika au kuhuisha mkataba wako wa upangishaji au wa kupanga, basi unaweza kutamatisha mkataba wako kwa kwa kumpatia mwenye nyumba wako:

- Tangazo la maandishi la utamatishaji ambao lazima uwe na tarehe ya kuanza kutumika kwenye tangazo. Tarehe ya kuanza kutumika lazima iwe angalau siku 30 baada ya mwenye nyumba kupokea tangazo hilo.
- Nakala ya amri ya ulinzi halali.

**Amri za Ulinzi za Muda Mrefu Zilizopatikana Kabla ya Kuingia Kwenye au Kuhuisha Mkataba wa Upangishaji au wa Kupanga**

Ikiwa ulipata amri yako halali ya ulinzi kabla ya kuingia kwenye au kuhuisha mkataba wa upangishaji au wa kupanga, basi unaweza kutamatisha mkataba wako kwa kutoa kwa mwenye nyumba wako:

- Tangazo la maandishi la utamatishaji ambao lazima uwe na tarehe ya kuanza kutumika kwenye tangazo. Tarehe ya kuanza kutumika lazima iwe angalau siku 30 baada ya mwenye nyumba kupokea tangazo hilo.
- Nakala ya amri ya ulinzi halali.
- Tatizo la usalama wako lililoongezeka baada ya kuingia au kuhuisha mkataba wa upangishaji au kupanga.

**Utamatishaji wa Upangishaji**

Mara baada ya mkataba wa upangishaji au wa kupanga kutamatishwa:

- Utawajibika tu kisheria kulipa kodi iliyo kwenye mkataba wako wa upangishaji au wa kupanga hadi tarehe ya utamatishaji itakapofika.
- Hutapata sifa mbaya, kuambiwa una tabia mbaya, au kuwajibika kisheria kulipa nyongeza ya kodi au ada kwa sababu tu ya utamatishaji wa mapema wa mkataba wa upangishaji au wa kupanga.
- Ikiwa mkataba wako wa upangishaji au wa kupanga utatamatishwa angalau siku 14 kabla ya kuhamia, basi hutatakiwa kulipia uharibifu au adhabu.

Kentucky Coalition
Against Domestic Violence
KCADV

# Kentucky's Domestic Violence Shelter Programs


**Kentucky Coalition Against Domestic Violence**
111 Darby Shire Circle
Frankfort, KY 40601
Phone: 502-209-5382
Fax: 502-226-5382
www.kcadv.org


**Domestic Violence Hotline**
(800) 799-SAFE(7233)




**The Ion Center**
Northern Kentucky
(859) 491-3335 (text enabled)

**GreenHouse17**
Lexington
(800) 544-2022

**The Ion Center**
Buffalo Trace
(606) 564-6708 (text enabled)

**The Center for Women & Families Crisis**
Louisville
(844) 237-2331

**DOVES of Gateway**
Morehead
(800) 221-4361

**SpringHaven, Inc.**
Elizabethtown
(800) 767-5838

**Owensboro Area Shelter & Information Services (OASIS)**
Owensboro
(800) 882-2873

**Safe Harbor**
Ashland
(800) 926-2150

**Turning Point Domestic Violence Services**
Prestonsburg
(800) 649-6605

**LKLP Safehouse**
Hazard
(800) 928-3131

**Merryman House**
Paducah
(800) 585-2686

**Sanctuary, Inc.**
Hopkinsville
(800) 766-0000

**Barren River Area Safe Space (BRASS)**
Bowling Green
(800) 928-1183

**Bethany House Abuse Shelter, Inc.**
Somerset
(800) 755-2017

**Cumberland Valley Domestic Violence Services**
London
(800) 755-5348

Administrative Office of the Courts
1001 Vandalay Drive
Frankfort, Kentucky 40601
800-928-2350 au 502-573-2350
www.kycourts.gov

P-123, Imechapishwa kwa Gharama za Jimbo, Toleo la Februari 2025